**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**

**S.L.P. 588,**
**54201 Mbozi - Songwe.**
**Simu:(025) 2580226Nukushi: (025) 2580213**
**Baruapepe:rbcsongwe@pccb.go.tz**
**Wavuti:http://www.pccb.go.tz**

**SONGWE APRILI ,2022**

# TAKUKURU YATOA MAFUNZO KWA WALIMU WALEZI WA SKAUTI

**Ndugu WanaHabari,**

Ninawasalimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Nimewaita hapa siku hii ya leo kwa ajili ya kuuhabarisha umma kupitia kuhusu Utendaji Kazi wa Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Songwe kwa kipindi cha Januari - Machi, 2022.

**Ndugu WanaHabari,**

## ELIMU KWA UMMA

Katika kipindi husika, ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Songwe kupitia Ofisi ya Mkoa pamoja na Wilaya zake, ilitoa elimu kwa Walimu kwa Walezi wa Skauti wa shule za Msingi na Sekondari, lengo likiwa ni kuwajengea uwezo katika utekelezaji wa Mpango wa TAKUSKA ambao ni Mkakati wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) na Chama cha Skauti Tanzania (CST) katika kuzuia na kupambana na rushwa nchini.

Vilevile, ofisi yetu ilishiriki kwenye Maadhimisho ya Wiki ya Sheria yaliyofanyika tarehe 24.03.2022 hadi 01.04.2022 kwa kutoa Elimu ya makosa ya Rushwa yaliyopo chini ya Sheria ya Kuzuia na kupambana na Rushwa Na. 11/2007 kwa Wanachama wa Klabu za Wapinga rushwa shule

ya Msingi Chapwa pamoja na Shule ya Sekondari Hollywood, Kufanya Mkutano wa Hadhara mmoja pamoja na kuweka Banda la Maonesho la kazi za TAKUKURU katika eneo la Kisimani Halmashauri ya Mji wa Tunduma.

Katika kipindi husika, ofisi yetu ilishiriki kwenye Maadhimisho ya Siku ya Wanawake duniani yaliyofanyika kimkoa tarehe 08.03.2022 wilayani Ileje kwa kutoa elimu kwa wananchi kwa njia ya onesho. Aidha kila Ofisi zetu za wilaya zilishiriki kwenye maadhimisho kiwilaya yaliyofanyika tarehe 07.03.2022 kwa kila wilaya kutoa Elimu kwa wananchi kwa njia ya onesho na kugawa vipeperushi. Kazi nyingine ni pamoja na: Uimarishaji wa Klabu za Wapinga rushwa 20; Semina 6; Kuelimisha umma kupitia vipindi vya Redio 4 pamoja na Mikutano ya hadhara 3.

**Ndugu WanaHabari,**

**Uzuiaji Rushwa**

Katika kipindi husika, Dawati la Uzuiaji Rushwa ambalo hufanya Chambuzi za Mifumo ya Taasisi na Idara mbalimbali za Serikali kwa lengo la kuzuia mianya ya Rushwa inayojitokeza kwenye mifumo ya kiutendaji pamoja kutembelea na kufanya ukaguzi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kushirikiana na wadau pamoja na wananchi ambao ndio wanufaika wa miradi husika, lilifanya kazi zifuatazo:

- Uchambuzi ya mfumo wa utendaji kazi wa TAMESA
- Kutembelea na kukagua utekelezaji wa jumla ya miradi ya maendeleo **minne** yenye thamani ya Shs. 887,293,500.00. Miradi hii imekaguliwa kwa kushirikiana na Wataalamu wa utekelezaji wa miradi, wadau pamoja na wananchi ambao ndio wanufaika wa miradi husika.

Matokeo ya miradi hiyo iliyokaguliwa ni kama ifuatavyo:

- Mradi wa ujenzi wa barabara ya Mbewe – Iyula kwa kiwango cha Changarawe wenye thamani ya Shs. 500,000,000.00. Mradi unaendelea vizuri

- Mradi wa ujenzi wa Zahanati ya Mtunduru wenye thamani wa Shs. 58,722,500.00 /=. Mradi umebainika kutotekelezwa kwa ubora kutokana na kutokuwepo kwa usimamizi madhubuti tkuoka kwa Wataalam wa Halmashauri

- Mradi wa ujenzi wa majosho matatu katika kata ya Mkulwe, Nzoka na Mkomba wenye thamani ya Shs. 54,000,000,000.00. Changamoto katika mradi huu ni wazabuni kutaka kulipwa fedha za vifaa vya ujenzi kabla ya kutoa huduma kwa Halmashauri hali iliyopelekea mradi kutokamilika kwa wakati.

- Mradi wa kufungua barabara tano katika kata ya Kapele chini ya TARURA wenye thamani ya Shs. 274,571,000.00. Mradi unaendelea vizuri

**Ndugu Wanahabari,**

**Katika Uchunguzi,** ofisi yetu ilipokea jumla ya taarifa **53** za malalamiko ya uwepo wa vitendo vya rushwa. Kati ya malalamiko hayo, malalamiko **44** yalihusu Rushwa na malalamiko **09** hayakuhusu rushwa hivyo watoa taarifa walipewa ushauri. Taarifa **44** zilizohusu rushwa zilifunguliwa majalada ya kuanzisha uchunguzi ambapo taarifa **29** uchunguzi wake bado unaendelea na taarifa **15** uchunguzi wake umekamilika na kufungwa kwa kuwa haukuweza kuthibitisha tuhuma. Hakuna taarifa zilizohamishiwa idara nyingine.

Mchanganuo wa malalamiko hayo kisekta yaliyopokelewa ni kama ifuatavyo: Malalamiko 25 yalihusu Idara ya Afya; Malalamiko 10 yalihusu Serikali za Vijiji na Kata Malalamiko 6 yalihusu Idara ya Elimu; Malalamiko 3

yalihusu Idara ya Fedha; Malalamiko 3 yalihusu Idara ya Utawala; Malalamiko 2 yalihusu Sekta binafsi ; Malalamiko 2 yalihusu Jeshi la Polisi; Lalamiko 1 lilihusu Idara ya Kilimo; Lalalamiko 1 lilihusu Idara ya Maji.

Katika kipindi husika pia kesi mpya 05 zilifunguliwa mahakamani na kufanya jumla ya kesi zinazoendelea kuwa 17, kesi 07 ziliamuliwa ambapo kesi 04 washitakiwa walitiwa hatiani, kesi 03 washtakiwa hawakukutwa na hatia na kesi 12 zinaendelea kusikilizwa mahakamani.

**Ndugu Wanahabari,**

**Kwa kipindi cha Aprili - Juni, 2022**, ofisi yetu imejipanga kutoa **elimu ya rushwa** kupitia vipindi vya Redio na TAKUKURU INAYOTEMBEA Kuelimisha umma kuhusu umuhimu wa kusimamia Miradi ya Maendeleo. Vile vile, Ofisi yetu kwa kipindi husika imejipanga kuendelea kufuatilia miradi ya maendeleo inayoendelea kutekelezwa katika mkoa wetu.

**Ndugu Wanahabari,**

Nitoe wito kwa wote wenye dhamana ya kutekeleza, kufuatilia na kusimamia miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika mkoa wa Songwe, kuhakikisha kuwa wanatekeleza majukumu yao kwa weledi na kuhakikisha kuwa wananchi wananufaika na miradi inayotekelezwa katika maeneo yao kama ilivyokusudiwa na serikali.

Mapambano dhidi ya Rushwa ni yetu sote hivyo kila mmoja atimize wajibu wake.

***Imetolewana:***

***Edings Mwakambonja,***
***Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Songwe***
***0738150214***